04

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR,

# APRILI, 2024

24 MEI, 2024

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI, 2024

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA


Jumla ya matukio 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Aprili, 2024 ambapo waathirika walikuwa 148. Waathirika wengi (waathirika 128) walikuwa watoto sawa na asilimia 86.5, wanawake walikuwa 16 sawa na asilimia 10.8 na wanaume walikuwa waathirika wanne (asilimia 2.7).
Miongoni mwa watoto (waathirika 128), wasichana walikuwa 108 (asilimia 84.4) na wavulana walikuwa 20 (asilimia 15.6).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Aprili 2024**



Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 77, ambapo waathirika 70 walikuwa wasichana na saba (7) walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 13 ambapo waathirika 12 walikuwa wavulana na mmoja (1) ni mwanamme. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni wanne (4) ambapo waathirika wote walikuwa wasichana. Matukio ya kutorosha ni saba(7) ambapo waathirika sita(6) walikuwa wasichana na mmoja(1) alikuwa mwanamke. Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 19 kati ya hayo, waathirika 15 walikuwa wasichana , watatu(3) walikuwa wanawake na mmoja alikuwa mvulana. Matukio ya shambulio yalikuwa 28 ambapo waathirika 13 walikuwa wasichana, saba(7) walikuwa wavulana, watano (5) walikuwa wanawake na watatu (3) walikuwa wanaume.


**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio, Aprili, 2024**




Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 40) sawa na asilimia 27.0 ikifuatia wilaya ya Mjini ambapo yameripotiwa matukio 34 (asilimia 23.0).

Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, tukio moja(1) sawa na asilimia 0.7 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Aprili, 2024**




Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 18.4 kufikia matukio 148 mwezi wa Aprili, 2024 kutoka matukio 125 kwa mwezi wa Machi, 2024. Aidha, matukio yote yameripotiwa kuongezeka isipokuwa matukio ya kuingilia kinyume na maumbile na Shambulio

Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya nyengine (matukio 40) kwa mwezi wa Aprili, 2024 na mwezi wa Machi, 2024 (matukio 38).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Machi, 2024 na Aprili, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 3 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 2 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 11 | 4 | 9 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 25 | 34 | 10 | 13 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 3 | 3 | 12 | 12 |
| Magharibi 'A' | 38 | 40 | 17 | 19 | 2 | 3 | 3 | 0 | 1 | 1 | 4 | 8 | 11 | 9 |
| Magharibi 'B' | 34 | 31 | 20 | 16 | 2 | 3 | 1 | 1 | 3 | 1 | 2 | 3 | 6 | 7 |
| Wete | 6 | 10 | 5 | 7 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 4 | 10 | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **125** | **148** | **67** | **77** | **8** | **13** | **6** | **4** | **4** | **7** | **11** | **19** | **29** | **28** |

Idadi ya matukio kwa mwaka hakukuwa na ongezeka la matukio. Jumla ya matukio 148 yaliyoripotiwa kwa mwezi Aprili, 2024 na mwezi wa Aprili, 2023. Matukio ya kulawiti/Kunajisi na shambulio la aibu /Kukashifu yameripotiwa kupungua kwa mwezi wa Aprili 2024.

Wilaya ya Magharibi “A” imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Aprili, 2024 (matukio 40) ambapo wilaya ya Mjini iliongoza kwa mwezi wa Aprili 2023 (matukio 37).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Aprili 2023 na Aprili, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 3 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 10 | 2 | 6 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 |
| Kati | 9 | 11 | 4 | 9 | 0 | 2 | 3 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 37 | 34 | 14 | 13 | 7 | 4 | 0 | 2 | 1 | 0 | 3 | 3 | 12 | 12 |
| Magharibi 'A' | 35 | 40 | 19 | 19 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 4 | 8 | 10 | 9 |
| Magharibi 'B' | 26 | 31 | 13 | 16 | 4 | 3 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 7 | 7 |
| Wete | 6 | 10 | 3 | 7 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 6 | 3 | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 10 | 4 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **148** | **148** | **72** | **77** | **20** | **13** | **4** | **4** | **4** | **7** | **16** | **19** | **32** | **28** |

Miongoni mwa watoto 128 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 70, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 12, Kuingilia kinyume na maumbile ni wasichana 4, Kutorosha walikuwa wasichana sita (6), shambulio la aibu walikuwa 16 kati yao wasichana walikuwa 15 na mvulana mmoja (1) na shambulio walikuwa 20 kati yao wasichana walikuwa 13 na wavulana walikuwa saba (7).

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Aprili, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 10 | 9 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 27 | 11 | 4 | 2 | 0 | 0 | 3 | 0 | 4 | 3 |
| Magharibi 'A' | 34 | 17 | 3 | 0 | 0 | 0 | 6 | 0 | 6 | 2 |
| Magharibi 'B' | 27 | 14 | 3 | 1 | 1 | 0 | 3 | 0 | 3 | 2 |
| Wete | 10 | 7 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 4 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **128** | **70** | **12** | **4** | **6** | **0** | **15** | **1** | **13** | **7** |

Miongoni mwa wanawake 16 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa 7, kutorosha alikuwa mwanamke mmoja (1), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa watatu (3) na shambulio walikuwa wanawake watano (5).

**Jadweli 1.4a: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Aprili, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Magharibi 'A' | 6 | 2 | 0 | 1 | 2 | 1 |
| Magharibi 'B' | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **16** | **7** | **0** | **1** | **3** | **5** |

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Aprili, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **4** | **1** | **0** | **0** | **3** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 74) sawa na asilimia 57.8 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio30) sawa na asilimia 23.4. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 54) sawa na asilimia 77.1 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri Aprili, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili naUdhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 0 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| 6-10 | | 4 | 5 | | | 1 | 0 | 1 | 1 | 7 | 1 | 3 | 23 |
| 11-14 | | 12 | 5 | | | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 7 | 30 |
| 15-17 | | 54 | 2 | | | 2 | 0 | 5 | 0 | 4 | 4 | 3 | 74 |
| **Jumla** | | **70** | **12** | | | **4** | **0** | **6** | **1** | **15** | **7** | **13** | **128** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Aprili, 2024 yameongezeka kwa asilimia 25.5 kufikia matukio 128 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka 102 kwa mwezi wa Machi 2024. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yameongeza isipokuwa umri wa miaka 0-5.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Mwezi Machi 2024 na Aprili 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Machi 2024 | Jumla Aprili 2024 |
| | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | | |
| 0-5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 4 | 1 | 0 | 0 | 8 | 1 |
| 6-10 | 4 | 4 | 5 | 5 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 8 | 4 | 4 | 16 | 23 |
| 11-14 | 15 | 12 | 2 | 5 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 3 | 6 | 9 | 26 | 30 |
| 15-17 | 39 | 54 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 5 | 1 | 4 | 8 | 7 | 52 | 74 |
| **Jumla** | **60** | **70** | **8** | **12** | **4** | **4** | **3** | **6** | **9** | **16** | **18** | **20** | **102** | **128** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 1.5 kufikia matukio 128 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka matukio 130 kwa mwezi wa Aprili 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa makundi yote yameripotiwa kupungua kwa mwezi Aprili, 2024 isipokuwa umri wa miaka 15-17.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Mtukio, Mwezi Aprili, 2023 na Aprili, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Aprili 2023 | Jumla Aprili 2024 |
| | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | | |
| 0-5 | 7 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 15 | 1 |
| 6-10 | 2 | 4 | 8 | 5 | 0 | 1 | 1 | 1 | 6 | 8 | 4 | 4 | 21 | 23 |
| 11-14 | 20 | 12 | 4 | 5 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 | 8 | 9 | 33 | 30 |
| 15-17 | 40 | 54 | 3 | 2 | 2 | 2 | 3 | 5 | 5 | 4 | 8 | 7 | 61 | 74 |
| **Jumla** | **69** | **70** | **19** | **12** | **3** | **4** | **4** | **6** | **15** | **16** | **20** | **20** | **130** | **128** |

Matukio mengi (matukio 61) yametokea Nyumbani kwa Mtuhumiwa sawa na asilimia 41.2 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) (matukio 58) sawa na asilimia 39.2 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Aprili, 2024**





Matukio 93 kati ya matukio 148 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 62.8 , matukio 35 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 23.6 na matukio 14 yapo mahakamani sawa na asilimia 9.6.

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Aprili, 2024**

| Aina ya Matukio | Idadi ya Matukio | Waathirika | | | | Hatua Zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | W'ume | W'ke | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 77 | | 7 | 70 | | 13 | 0 | 0 | 0 | 20 | 40 |
| Kulawiti | 13 | 1 | | | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 9 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 4 | | 0 | 4 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 |
| Kutorosha | 7 | 0 | 1 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 19 | 0 | 3 | 15 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 15 |
| Shambulio | 28 | 3 | 5 | 13 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 19 |
| **Jumla** | **148** | **4** | **16** | **108** | **20** | **14** | **0** | **0** | **0** | **35** | **93** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Aprili 2024 walikuwa 148 kati yao, 115 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 77.7, 31 walikuwa jirani sawa na asilimia 20.9, wawili(2) walikuwa wapenzi sawa na asilimia 1.4.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Aprili, 2024**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR APRILI 2024

Jumla ya Majalada 65 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Aprili 2024, ambayo yalihusisha makosa 71.
Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 49) sawa na asilimia 69 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine ambapo ilikuwa na idadi ya makosa chini ya kumi yaliyopokelewa.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Aprili,2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 6 | 9 |
| Kusini Unguja | 4 | 5 |
| Mjini Magharibi | 47 | 49 |
| Kaskazini Pemba | 6 | 6 |
| Kusini Pemba | 2 | 2 |
| **Jumla** | **65** | **71** |

Kati ya Majalada 65 yaliyopokelewa, majalada 9 yamependekezwa kufungwa, majalada 13 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 12 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada 31 hayajatolewa uamuzi.

**Jadweli 2.2: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Aprili 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalio ruhusiwa kwenda Mahakamani | Yalio Pendekezwa kufungwa | Yalio rudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 6 | 1 | 0 | 0 | 5 |
| Kusini Unguja | 4 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Mjini Magharibi | 47 | 6 | 8 | 11 | 22 |
| Kaskazini Pemba | 6 | 3 | 1 | 1 | 1 |
| Kusini Pemba | **2** | **2** | **0** | **0** | **0** |
| **Jumla** | **65** | **12** | **9** | **13** | **31** |

Miongoni mwa makosa 71 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 34) sawa na asilimia 47.9 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Aina ya Makosa, Aprili 2024**

| Mkoa | Idadi ya Makosa | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kulawiti/Kunajis | Kutorosha | Shanbulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio | Kuteleke za mtoto |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 9 | 4 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Unguja | 5 | 3 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 49 | 21 | 11 | 8 | 2 | 6 | 0 | 1 |
| Kaskazini Pemba | 6 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **71** | **34** | **12** | **10** | **7** | **7** | **0** | **1** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI 2024

Jumla ya mashauri 17 yamefunguliwa katika mahkama za Udhalilishaji kwa mwezi wa Aprili, 2024 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 10) sawa na asilimia 58.8 ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Machi, 2024**




Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika mahkama za udhalilishaji Zanzibar ni 17. Ambapo mashauri matano (5) yametolewa uamuzi na mashauri 12 bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Aprili, 2024**

| Aina ya Kosa | Zilizofungu liwa | Zilizotolewa uamuzi | | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|
| | | Limefutwa | Faini | |
| Kubaka | 2 | 0 | 2 | 0 |
| Kulawiti | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 10 | 0 | 0 | 10 |
| Kutorosha | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 3 | 0 | 2 | 1 |
| **Jumla** | **17** | **1** | **4** | **12** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 17 ambapo washtakiwa 16 walikuwa wanaume na mmoja(1) alikuwa mwanamke. Washtakiwa wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 22-25 (washtakiwa 6) sawa na asilimia 35.2.

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 17 ambapo waathirika wawili (2) walikuwa wavulana na waathirika 15 walikuwa ni wasichana na wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 10-14 (waathirika 8) sawa na asilimia 47.1.

**Jadweli 3.2: Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Aprili, 2024**

| Umri wa Mshtakiwa | Jinsi za Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Jinsi za Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| 14-17 | 3 | 0 | 0-4 | 1 | 0 |
| 18-21 | 5 | 0 | 5-9 | 1 | 1 |
| 22-25 | 6 | 0 | 10-14 | 0 | 8 |
| 26-29 | 1 | 0 | 15-19 | 0 | 6 |
| 30-33 | 1 | 1 | 20-24 | 0 | 0 |
| 34-37 | 0 | 0 | 25-29 | 0 | 0 |
| 38-41 | 0 | 0 | 30-34 | 0 | 0 |
| 42-45 | 0 | 0 | 42-45 | 0 | 0 |
| 46-49 | 0 | 0 | 46-49 | 0 | 0 |
| 50+ | 2 | 0 | 50+ | 0 | 0 |
| **Jumla** | **16** | **1** | **Jumla** | **2** | **15** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 148 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Aprili, 2024 ambapo waathirika walikuwa 148 Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 40) sawa na asilimia 27.0.  Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 18.4 kufikia matukio 148 mwezi wa Aprili, 2024 kutoka matukio 125 kwa mwezi wa Machi, 2024.

Matukio 93 kati ya matukio 148 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la  Polisi  sawa na asilimia 62.8 ,  matukio 35 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 23.6 na matukio 14 yapo mahakamani sawa na asilimia 9.6.

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Aprili, 2024**

| Eneo la Matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia Kinyume naMaumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 5 | [redacted] | 5 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 29 | [redacted] | 29 | [redacted] | 1 | 1 | 1 | [redacted] | 1 | 7 | 0 | 7 | 6 | 0 | 6 | 11 | 6 | 17 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 7 | [redacted] | 7 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 11 | [redacted] | 11 | [redacted] | 4 | 4 | 1 | [redacted] | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 25 | [redacted] | 25 | [redacted] | 8 | 8 | 2 | [redacted] | 2 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 12 | 7 | 4 | 11 |
| **Jumla** | **77** | [redacted] | **77** | [redacted] | **13** | **13** | **4** | [redacted] | **4** | **7** | **0** | **7** | **18** | **1** | **19** | **18** | **10** | **28** |

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio baina ya Mwezi Machi, 2024 na Aprili, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 |
| Nyumbani kwa Muathirika | 7 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 10 | 0 | 20 | 5 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 18 | 29 | 2 | 1 | 3 | 1 | 2 | 7 | 5 | 6 | 8 | 17 | 38 | 61 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 3 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 7 |
| Sehemu za kazi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 15 | 11 | 1 | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 3 | 0 | 22 | 17 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 24 | 25 | 5 | 8 | 2 | 2 | 1 | 0 | 2 | 12 | 8 | 11 | 42 | 58 |
| **Jumla** | **67** | **77** | **8** | **13** | **6** | **4** | **4** | **7** | **11** | **19** | **29** | **28** | **125** | **148** |

Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Aprili, 2024

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 11 | 9 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 34 | 13 | 4 | 2 | 0 | 3 | 12 |
| Magharibi 'A' | 40 | 19 | 3 | 0 | 1 | 8 | 9 |
| Magharibi 'B' | 31 | 16 | 3 | 1 | 1 | 3 | 7 |
| Wete | 10 | 7 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Micheweni | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 10 | 4 | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 |
| Mkoani | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| **Zanzibar** | **148** | **77** | **13** | **4** | **7** | **19** | **28** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Machi, 2024 na Aprili, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 |
| Kubaka | 67 | 77 | 7 | 7 | 60 | 70 | | | | |
| Kulawiti | 8 | 13 | | | | | 8 | 12 | 0 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 4 | 2 | 0 | 4 | 4 | | | | |
| Kutorosha | 4 | 7 | 1 | 1 | 3 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 11 | 19 | 2 | 3 | 9 | 15 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 29 | 28 | 5 | 5 | 8 | 13 | 10 | 7 | 6 | 3 |
| **Jumla** | **125** | **148** | **17** | **16** | **84** | **108** | **18** | **20** | **6** | **4** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Aprili, 2023 na Aprili, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 |
| Kubaka | 72 | 77 | 5 | 7 | 69 | 70 | | | | |
| Kulawiti | 20 | 13 | | | | | 19 | 12 | 2 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 4 | 4 | 1 | 0 | 3 | 4 | | | | |
| Kutorosha | 4 | 7 | 0 | 1 | 4 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 16 | 19 | 2 | 3 | 14 | 15 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Shambulio | 32 | 28 | 8 | 5 | 9 | 13 | 11 | 7 | 4 | 3 |
| **Jumla** | **148** | **148** | **16** | **16** | **99** | **108** | **31** | **20** | **6** | **4** |

**Jadweli 5.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea Aprili, 2024**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajis | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 03:01 - 06:00 Mchana | 11 | 3 | 1 | 1 | 6 | 3 | 25 |
| 06:01 - 09:00 Jioni | 11 | 3 | 0 | 1 | 7 | 7 | 29 |
| 09:01 - 12:00 Jioni | 18 | 5 | 2 | 3 | 4 | 8 | 40 |
| 12:01 - 03:00 Usiku | 27 | 2 | 1 | 2 | 2 | 6 | 40 |
| 03:01 - 06:00 Usiku | 8 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 12 |
| 06:01 - 09:00 Usiku | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **77** | **13** | **4** | **7** | **19** | **28** | **148** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136
MMP, Zanzibar.